



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA HANDENI
MTIHANI WA PAMOJA NUSU MUHULA KIDATO CHA I
MEI 2025



MSIMBO: 021
Muda: Saa 2:30

KISWAHILI
MsomiBora.com
MAELEKEZO

- Mtihani huu una sehemu A, B na C, wenye jumla ya maswali saba (7).
- Jibu maswali yote.
- Sehemu A ina jumla ya alama kumi na tano (15), sehemu B ina jumla ya alama arobaini na nne (44) na sehemu C ina jumla ya alama arobaini na moja (41).

SEHEMU A(Alama 15)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Katika kipengele(i) —(x)andika herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku
 - i. Tungo ipi kati ya zifuatazo inafafanua maana ya lugha ?

A)Lugha ni utambulisho wa jamiii

B)Lugha ni sauti za Nasibu zenye maana

c)Lugha ni kiungo muhimu katika mawasiliano

D)Lugha huleta migogoro katika jamii
 - ii. Vipengele vipi kati ya vifuatavyo vinabainisha utamaduni wa Mtanzania?

A)Unasibu,salamu na mavazi

B)Vyakula ,kilimo na mavazi

c)Salamu,vyakula na mavazi

D)Nyimbo,unasibu na mavazi
 - iii. Ipi kati ya zifutazo ni fursa itokanayo na lugha ya kiswahili?

A)kuwatambulisha watu

B)kuwafundisha watu wa mataifa mengine

C)kuburudika

D)kuweza kuelewana vizuri
 - iv. Kanuni na taratibu znazotumiwa na wazungumzaji

A)Sarufi

B)lugha

C)Mawasiliano

D)Utamaduni
 - v. Huhusika na namna vitamkwa vya lugha vinavyotamkwa,pamoja na mahali pakutamkia,

A)Sarufi maumbo

B)Sarufi miundo

C)Sarufi maana

D)Sarufi matashi
 - vi. Je ni kipi tunaweza kufanya ili kulinda na kuhifadhi utamaduni wetu?

A)Kutambua na kulinda rasilimali,mazingira na urithi wa utamaduni

B)kufundisha kiswahili kwa wageni

C)Kuvaa mavazi ya kiswahili

D)kusoma somo la kiswahili
 - vii. Kundi la kamusi zinazoandikwa kwa lugha moja,

A) mahuliti

B) wahidiya

C) Thania

D) Tarbia

viii. Je, lugha inamuhusu nani?

A) Binadamu B) wanyama C) Ndege D) Wadudu

ix. Kundi la nomino za pekee

A) dawati, kisu, kikombe, Tanga na Dodoma B) Mungu, Asha kiti, meza, na kikombe

C) wadudu, wanyama ndege na binadamu D) Asha, Maria, Kenya na Uganda

x. Ni maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu majina na viwakilishi vyake

A) Vivumishi B) Vielezi C) Vitenzi D) Viunganishi

i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix	x

2. Oanisha maneno ya Orodha A pamoja na Orodha B kisha andika jibu sahihi kwenye nafasi uliyopewa

ORODHA A	ORODHA B
i) hutoa taarifa juu ya linavyofanyika, namna linavyofanyika, muda pamoja na mahali	A) NOMINO
ii) Hueleza au kutoa taarifa zaidi juu ya Nomino na kiwakilishi	B) VIWAKILISHI
iii) Huonesha tendo linalotendeka	C) VIVUMISHI
iv) Huonesha hali au tabia fulani, iliyopo au isiyokuwepo	D) VIHUSISHI
v) Huonesha hisia, kama vile furaha, huzuni n.k	E) VIELEZI
	F) VIHISISHI
	G) VIUNGANISI
	H) VITENZI

ORODHA A	i	ii	iii	iv	v
ORODHA B					

SEHEMU B (Alama 41) Jibu maswali yote

3..a) Sentensi zifuatazo zina makosa, ziandike kwa usahihi

i) Nipatie fiatu fyangu tafasali.....

- ii) Baba amenunua mbuzi.....
- iii) Rehema amekwenda Ilinga.....
- iv) Tulipomariza kula, tulirara.....
- v) Nimekuelewa barabara.....

b) Tunga sentensi kwakutumia vipashio vifuatavyo

- i) N+V+T.....
- II) W+T.....
- III) T+E.....
- IV) W+TS+TS+T+U+N+T.....
- V) N+T+E.....

4. Taja kwa mifano aina zote za vivumishi.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

5.a) Kamusi ni nini?

.....

.....

b) Wewe ni kiongozi wa kidato cha kwanza mkondo A, umepewa majina yafuatayo, yapange kama yatakavyoonekana kwenye daftari la mahudhurio

i) Aria ii) Aidhati iii) Athumani iv) Aliya v) Askari vi) Ashura, vii) Aisha viii) Abdi ix) Awazi x) Agnes

.....

.....

SEHEMU C (Alama 44)

Jibu maswali yote

6.a) Je wewe kama mwanafuzi wa kidato cha kwanza wa somo la kiswahili, kamusi ina umuhimu gani kwako? (taja hoja tano)

i)

ii)

iii)

iv)

v)

b) Je, lugha ya kiswahili imepewa hadhi gani kimataifa? (taja hoja tano)

i)

ii)

iii)

iv)

v)

c) Taja mambo matano yakuzingatia katika kusoma kwa ufasaha

i)

ii)

iii)

iv)

v)

7. a) John ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Keryo. John hajui ufahamu una maanisha nini, wewe kwakua umesoma kuhusu ufahamu, msaidie John kujua fasili ya ufahamu,

.....
.....

b) Umuhimu wa ufahamu katika maisha yake ya kila siku (hoja tano)

i)

ii)

iii)

iv)

v)